FORM FOUR TERM ONE EXAM 2017

KISWAHILI
Karatasi 2
Lugha
Muda: Saa 2½

SCHOOLS NET KENYA
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU A: UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

Halmashauri ya mpwito nchini imetoa mwongozo kuhusu majukumu yanayofaa kutekelezwa na serikali za kaunti kote nchini kuanzia Julai mosi mwaka huu.

Mwongozo huo utasaidia kuondoa wasiwasi ambao baadhi ya mashirika yasiyo ya serikali yalielezea kuwa huenda baadhi ya sekta zisipate ufadhili kutokana na utata kuhusu ni serikali ipi inafaa kuzishughulikia.

Shughuli hizi zinajumuisha kilimo ambapo zitahakikisha maendeleo ya mimea,mifugo na uvuvi. Serikali za kaunti pia zitashughulikia huduma za afya kuhakikisha kuna dawa na vifaa vya kutosha katika zahanati na hospitali.

Uhifadhi wa mazingira na tamaduni za kijamii kama vile makavazi,maktaba na majumba ya burudani vilevile zitakuwa chini ya usimamizi wa kaunti.

Serikali hizo pia zitasimamia masuala ya uchukuzi kwa kushughulikia ukarabati wa barabara, taa za kudhibiti msongamano wa magari na bandari.

Kulingana na taarifa iliyochapishwa kwenye vyombo vya habari, serikali hizo pia zitashughulikia maendeleo ya biashara na vyama vya ushirika.

“Serikali za kaunti zitajihusisha na kudhibiti mipaka na matumizi ya kawi,elimu ya chekechea na vyuo vya ufundi katika ngazi za vijijini, taarifa hiyo ilisema.

Halmashauri hiyo ilisema kuwa serikali hizo zitasimamia uhifadhi wa misitu, ardhi, huduma za maji kupambana na mikasa ya moto, dawa za kulevya na picha za ngono.

Taarifa hiyo iliyotiwa sahihi na mwenyekiti wa Halmashauri ya Mpwito ilisema pia serikali za kaunti zinapaswa kuhakikisha kuwa umma umeshirikishwa katika usimamizi wa raslimali za vijiji.

Kulingana na kipengee cha 15 cha katiba ya Kenya, bunge la kitaifa katika muda usiopita miaka mitatu kutoka siku ya uchaguzi linahitajika kuunda sheria za kuhakikisha kuwa serikali za kaunti zimepata uwezo wa kuendeleza shughuli zake.

Aidha kipengee cha 23 kuhusu ugatuzi kinahitaji Halmashauri ya Mpwito kutambua shughuli zitakazo tengewa serikali za kaunti kutoka serikali kuu punde tu baada ya uchaguzi mkuu. Shughuli hizi zilitayarishwa kupitia hati ya sheria nambari 16 ya 2013.

Katiba katika kipengele cha 24 inatoa masharti ya kufuatwa kabla serikali za kaunti kuanza rasmi shughuli zake za kutoa huduma kwa wananchi.

Maswali

a) Yape makala haya kichwa mwafaka. (alama 1)

.....

.....

b) Je, kaunti inawajibikaje katika kuwahudumia wananchi? (alama 2)

.....

.....

c) Utawala wa kaunti unaweza kupunguza vipi maafa yanayotokea kutokana na mapuuza ya mwanadamu? (alama 3)

.....

.....

.....

.....

d) Bunge la kitaifa lina wajibu gani katika serikali ya kaunti? (alama 2)

.....

.....

.....

.....

e) Ni changamoto zipi zinazoweza kukabili suala la ugatuzi nchini? (alama 3)

.....

.....

.....

.....

f) Ni kwa njia gani serikali ya kaunti inaweza kufufua uchumi wa nchi na kuinua kiwango cha maisha ili kufikia ruwaza ya 2030 (alama 2)

.....

.....

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika ufahamu.

(i) Uchukuzi

.....

.....

(ii) Ugatuzi

.....

.....

UFUPISHO (ALAMA 15)

Teknolojia mpya ni tawi la maarifa linalohusiana na sayansi kwa upande mmoja na uhandisi (Uinjinia) kwa upande mwingine. Sayansi ni elimu inayotokana na uchunguzi na majaribio katika maabara. Nao uhandisi ni ujuzi wa kuunda mitambo. Maarifa ya sayansi yanapotumiwa kutengeneza vitu viwandani hali hii inakuwa teknolojia.

Zao mojawapo la teknolojia mpya ni simu tamba. Watu vijijini sasa wanawasiliana na jamaa zao walio mbali. Akina nyanya wanapopanda njugu, kupalilia migomba, kukama ngamia na kukuna nazi, wanaweza kuzungumza na wajukuu wao walio Uingereza, Uchina na kwingine kule. Hakuna mahali ambapo hapajafikiwa na teknolojia mpya. Tukitembea baadhi ya nyumba tutaona vifaa kama vile tanuri la miale au

mikrowavu ambalo linapika maharagwe yakaiva kwa dakika chache tu. Majokofu nayo yanatuwezesha kuhifadhi vyakula bila kuharibika. Hata maiti na mizoga inaweza kuhifadhiwa kwa miaka mingi kwa ajili ya utafiti bila kuoza katika ufuo wa mochari.

Kwa upande wa kilimo, teknolojia imefanya pakubwa. La kustaajabisha ni mtu mmoja kulima eneo kubwa la shamba kwa trekta. Halafu akapanda kwa tandazi, akanyunyizia dawa kunyausha magugu, akavuna na kukoboa mahindi akiwa pekee yake. Siku hizi inawezekana kukuza mimea na kufuga wanyama wanaokomaa kwa muda mfupi na kutoa mazao maradufu kwa sababu ya teknolojia mpya. Teknolojia imewezesha watu kuvumbua ama nyingi za nishati. Badala ya kutegemea umeme unaotokana na maji tu, sasa watu wanatumia mvuke, nguvu za upepo na nishati ya jua kupata umeme. Kwa sababu hii hata mababu zetu vijijini wanatazama televisheni bila shida au wahka.

Kwa upande mwingine, teknolojia ina madhara yake. Kwa mfano, uundaji wa silaha kali unaendelea kuwaangamiza watu wengi. Mabomu ya kitonoradi yaliyoangushwa Hiroshima na Nagasaki Japan mwaka wa 1945 ni zao la kisayansi. Haya yaliwaua watu wengi na madhara yake bado yanadhihirika hata leo katika maumbile ya watoto wanaozaliwa na upungufu. Tena magaidi na wahalifu wa kimataifa wanatumia teknolojia mpya kuimarisha mbinu zao za kutenda maovu. Isitoshe, inawezekana kutumia teknolojia kuagiza benki kutuma pesa nje ya nchi bila mwenye hazina kujua.

Wahalifu wanaweza kusikiza mawasiliano ya watu kwa simu hata ikiwa ni baina ya polisi. Kisha matatizo mengi ya kiafya yasemekana yanatokana na vyakula vilivyokuzwa kwa kutumia teknolojia mpya. Katika usafiri, kuna gari moshi lenye kutumia stima badala ya makaa. Hili ni zao la teknolojia mpya vilevile. Ingawa mwendo wake ni wa kasi, kasi hiyo na stima huweza kusababisha ajali mbaya mno.

Maswali

(a) Fupisha aya ya pili na ya tatu. (maneno 70-80) (alama 8) Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(b) Kwa kutumia maneno (55-65) Eleza mambo muhimu yanayoangaziwa kwenye aya ya 4 na 5 (alama7)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

SEHEMU C: SARUFI NA`` MATUMIZI YA LUGHA

(a) Bainisha sifa zinazotofautisha sauti zifuatazo. (alama 2)

/ e/na/ u/

.....

.....

.....

b)(i) Ainisha viambishi tamati katika tungo lifuatalo (alama 2)

Aliwalilia

.....

.....

(ii) Eleza maana ya mzizi. (alama 1)

.....

.....

(c) Pigia mstari silabi inayowekwa shadda katika tungo lifuatalo. (alama 1)

Alituchochea

.....

.....

(d) Eleza matumizi ya kiimbo. (alama 2)

.....

.....

(e) Tunga sentensi moja ukitumia kirejeshi kisisitizi cha karibu katika ngeli ya LI — YA umoja. (alama 2)

.....

.....

(f) Andika upya sentensi ifuatayo ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa nomino Mama alituimbia hadi tukafurahi. (alama 2)

.....

.....

(g) Ainisha vitenzi katika tungo lifuatalo. (alama 2)

Huyu alikuwa angali bwenini.

.....

.....

(h) Ainisha vivurnishi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mtoto wa jirani mwenye shamba kubwa anaimba.

.....

.....

(i) Tambua na ueleze aina\\ za vihusishi. (atama 2)

Mti ulioanguka karibu na darasa utachomwa hadi uishe.

.....

.....

(j) Onyesha chagizo katika tungo hili. (alama 1)

Mwalimu mnene zaidi anamiliki shamba lile kubwa.

.....

.....

(k) Tunga sentensi ukitumia nomino ifuatayo pamoja na kivumishi kisisitizi cha mbali kidogo,

Mgomba (ala 2)

.....

.....

(1) Tunga sentensi mbili ukitumia neno kisabuni kama: (ala 2)

(i) Nomino

.....

.....

(ii) kielezi

.....

.....

(m) Andika visawe vya (ala 2)

(i) Hidaya

.....

(ii) Ngeu

.....

(n) landike sentensi ifuatayo upya ukitumia ‘0” rejeshi tamati (ala 2)

Chumvi iliyochafuka si ile unayoizungumzia.

.....

.....

.....

(o) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo (ala 2)

Mwanasiasa shupavu aliyewachochea wananchi amekamatwa.

.....

.....

.....

(p) Yakinisha sentensi ifuatayo katika umoja (ala 2)

Nyuzi zisingekatika zisingepotea.

.....

.....

.....

(q) Nomino ‘huruma’ i katika ngeli gani? (ala 1)

.....

.....

.....

(r) Taja aina **mbili** za mofimu na uonyeshe mfano kwa kila. (a1a2)

.....

.....

.....

SEHEMU D: ISIMU JAMII

(a) Eleza rnaana ya istilahi zifuatazo za isimu jamli. (ala 2)

(i) Diglosia

.....

.....

(iii) Misimu

.....

.....

.....

(b)Taja na ueleze njia mbalimbali za kukuza msamiati wa Kiswahili. (ala.3)

.....

.....

.....

.....

(c)Eleza sifa **tatu** za sajili ya mahirimu. (ala. 5)

.....

.....

.....

.....

.....

.....